Tangazo La Serikali Na. 672 la tarehe 25/11/2022

SHERIA YA MIPANGOMIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA MPANGO WA URASIMISHAJI WA ENEO LA SHANWE YA MWAKA, 2022

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Mpango wa Urasimishaji wa Eneo la Shanwe ya Mwaka, 2022.

Kutangazwa kwa eneo la upangaji

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya urasimishaji.

Mpango wa kina wa eneo

3. Mpango wa kina wa eneo lililoainishwa katika Jedwali unaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda.

*Tangazo La Serikali Na. 672 (Linaendelea.)*

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la Mpango wa Urasimishaji lipo ndani ya Mipaka ifuatayo:

“Unaanzia kwenye alama ya mipaka ya upimaji namba ‘C1’ karibu na daraja la Kivukoni na mpaka wa Shanwe yenye majira - nukta 286097 E, 9300555 N, unaelekea Kaskazini - Magharibi uelekeo wa N46°05'26"W kando ya barabara ya Kasokola kwa umbali wa kilomita 0.466 hadi alama ya mpaka ya upimaji namba C2 yenye majira - nukta 285762 E, 9300878N), baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini Magharibi uelekeo wa N21°29'27"W kando ya barabara ya Kasokola kwa umbali wa kilomita 0.387 hadi alama ya mpaka ya upimaji namba C3 yenye majira - nukta 285620 E, 9301238 N, baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini Mashariki uelekeo wa N52°31'49"E kando ya barabara ya Kasokola kwa umbali wa kilomita 0.230 hadi alama ya mpaka ya upimaji namba C4 yenye majira - nukta 285802 E, 9301379 N, baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki uelekeo wa S71°45'38"E kwa umbali wa kilomita 0.194 hadi alama ya mpaka ya upimaji namba C5 yenye majira - nukta 285987 E, 9301318 N, baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki uelekeo wa S 81°50'51"E kwa umbali wa kilomita 0.044 hadi alama ya mpaka ya upimaji namba C6 yenye majira - nukta 286030 E, 9301324 N), baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki uelekeo wa S 37°01'26"E kwa umbali wa kilomita 0.415 hadi alama ya mpaka ya upimaji namba C7 mpaka wa Shanwe na Kivukoni yenye majira - nukta 286280 E, 9300993 N, baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi uelekeo wa S 22°40'17"E kwa umbali wa kilomita 0.475 hadi ulipoanzia kwenye alama ya mipaka ya upimaji namba C1 yenye majira - nukta 286097 E, 9300555 N”.

Dodoma,
8 Novemba, 2022

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*